**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**
(BARUA ZOTE ZIELEKEZWE KWA MKURUGENZI MTENDAJI)

Simu: 0282770020,
Nukushi: 0282770019,
Barua pepe: info@kishapudc.go.tz
Tovuti: www.kishapudc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P. 1288,
22Barabara ya DED-DC
**37582 KISHAPU.**

*Unapojibu Tafadhali Taja:-*

Kumb.Na.KDC.P.70/2/VOL.85 12/06/2025

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu amepokea Kibali kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kilichotoa idhini ya utekelezaji wa nafasi za Ajira mpya katika Ikama ya mwaka wa fedha 2024/2025 chenye Kumb.NaFA.97/228/01/A/25 cha tarehe 29 Aprili, 2025. Hivyo anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kutuma maombi katika nafasi zifuatazo:-

### 1.1 MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II ( NAFASI - 2)

#### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha nne au sita mwenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA Level 6 ya Uhazili. Aidha, awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 100 kwa dakika moja na kupata program za Kompyuta za ofisi kama vile: Word, Excel, powerpoint, internet, Email na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### 1.1.2 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, mihadi, wageni, tarehe ya vikao, safari za mkuu wake na ratiba ya kazi za kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anayofanyia kazi, kumtaarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.

v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maafisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

**1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS C.**

**1.2 WASAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA II (NAFASI 3)**

**1.2.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na Elimu ya kidato cha Nne (IV) au cha Sita (VI) aliehitimu mafunzo ya stashahada/Diploma (NTA Level 6) katika fani ya Utunzaji wa Kumbukumbu kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, wenye ujuzi wa kutumia kompyuta.

**1.2.2 KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kuorodhesha barua zinazoingia masijala kwenye regista (incoming correspondence register).
ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi (Outgoing Correspondence Register)
iii. Kusambaza majalada kwa Watendaji (Action Office).
iv. Kupokea majalada yanayorudi masijala kutoka kwa watendaji.
v. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka au majalada yanayohitajika na watendaji.
vi. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (Racks/Filling cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa.
vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani na nje ya Taasisi (File tracking).

**1.2.3 NGAZI YA MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS C.**

**1.3 DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 8)**

**1.3.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo wamefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika. Wawe wamehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.3.2 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (log book)
vi. Kufanya usafi wa gari.

### 1.3.3 NGAZI YA MSHAHARA.

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B.**

**MASHARTI YA JUMLA YA MWOMBAJI KAZI**

i. Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
ii. Awe hajawahi kufungwa wala kupatikana na hatia katika makosa yoyote ya jinai.
iii. Mwombaji mwenye cheti cha kughushi asijaribu kuomba nafasi hizi, endapo atabainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
iv. Awe hajawahi kufukuzwa kazi, kupunguzwa, kuachishwa au kustaafishwa kazi katika Utumishi wa Umma.
v. Mwombaji aambatishe vivuli vya vyeti vya Shule, Taaluma, Kuzaliwa na Kitambulisho vya Taifa (NIDA).
vi. Mwombaji wa kazi mwenye majina yaliyoongezeka au kutofautiana ahakikishe anakuwa kiapo (Deedpoll)
vii. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results" hati matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**
viii. Kwa mwombaji wa nafasi ya Dereva anatakiwa kuwa vyeti vilivyompa madaraja ya leseni ya Udereva.
ix. Muombaji aambatishe maelezo binafsi (CV).
x. Mwombaji aweke picha ndogo 1 ( passport size) iliyopigwa hivi karibuni katika ukurasa wa ajira portal.
xi. Mwombaji aandike kwa usahihi anwani yake na namba ya simu inayopatikana muda wote kwa ajili ya mawasiliano.
xii. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **27/06/2025.**

xiii. Kumbukuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu. Anuani ya barua hiyo ilekezwe kwa

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Walaya
22 Barabara ya DED-DC
S.L.P 1288,
**37582 KISHAPU.**

xii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anwani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz. (Anwani hii pia inapatikana kwenye tovuti Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa "Recruitment Portal").

xiii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika Tangazo hili **HAYATAFIKILIWA.**

**TAGANZO HILI LIMETOLEWA NA:-**

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KISHAPU